



“Tunataka kila mtu  
ajue kuwa anaweza  
kuchukua likizo ya  
ugonjwa yenye  
malipo, sio tu kwa  
sababu tu ni haki  
yake, ila kwa sababu  
kila mtu anastahili  
likizo hiyo.”

**Ed Gainey,  
Meya wa Pittsburgh**



Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea:  
[pittsburghpa.gov/mayor/paidsickleave](http://pittsburghpa.gov/mayor/paidsickleave)  
au tuma barua pepe kwa  
[paidsickleave@pittsburghpa.gov](mailto:paidsickleave@pittsburghpa.gov)


# LIKIZO YA UGONJWA YENYE MALIPO



kwa wafanyakazi wa  
Jiji la Pittsburgh

## JE, NITAPATA LIKIZO YA UGONJWA YENYE MALIPO

Wafanyakazi wa muda wote NA wa muda wanaofanya kazi kwa masaa 35+ kwa wiki kwa mwaka katika Jiji la the Pittsburgh wanastahiki kuchukua likizo ya Siku za Ugonjwa zenye Malipo. Ikiwa unapata PTO huenda tayari unakubali kuchukua likizo hii.



## JE, NITAJUA VIPI MUDA WANGU WA KULIPWA WAKATI WA UGONJWA?

Isipokuwa kama mwajiri huwa anatoa Likizo ya Ugonjwa yenye Malipo ya kila mwaka, wafanyakazi hupata angalau saa 1 ya muda wa kulipwa wakati wa ugonjwa kwa kila masaa 35 wanazofanya kazi Jijini.

# JUA HAKI ZAKO



## Je, ninaweza kuadhibiwa kwa kuchukua likizo yangu ya ugonjwa yenye malipo?

HAPANA. **Kulipiza kisasi kunakiuka sheria.** Waajiri hawawezi kukuadhibu kwa kutumia Siku za Ugonjwa zenye Malipo.




## Je, ninapaswa kufanya nini iwapo mwajiri wangu amekiuka haki yangu ya Likizo ya Ugonjwa yenye Malipo?

Tafadhali wasiliana nasi kwa [paysickleave@pittsburghpa.gov](mailto:paysickleave@pittsburghpa.gov).

## JE, NINaweza KUTUMIA MUDA WA LIKIZO YANGU YA UGONJWA YENYE MALIPO VIPI?

Wafanyakazi wanaostahiki wanaweza kutumia muda wao wa kulipwa wakati wa ugonjwa wanapokuwa wagonjwa, wanapohitaji kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu, au wanapohitaji matibabu. Wanaweza pia kutumia muda huo kuwatunza wanafamilia.



## JE, NITAPATA MUDA GANI WA LIKIZO YA UGONJWA YENYE MALIPO?

Waajiri walio na wafanyakazi 15+ lazima watoe masaa 40 kwa mwaka ya Likizo ya Ugonjwa yenye Malipo; waajiri wadogo lazima watoe masaa 24.